Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU Bulletin

*JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.22 - 2022*

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaendelea kuboresha Elimu yetu*



**MRADI WA BOOST**



# Serikali yafanya Maboresho Makubwa Miundombinu Vyuo vya Ualimu

## - KAZI IENDELEE -

www.moe.go.tz




**BODI YA UHARIRI**

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
***Kamishna wa Elimu***

Atupele Mwambene
***Mkurugenzi wa Sera na Mipango***

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

Nelly Mtema
***Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Ipyana Mwaipaja

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## Hivi ndivyo Mradi wa BOOST utakavyoimarisha Elimu ya Awali, Msingi

Tumeshuhudia maboresho makubwa yakifanywa na Serikali katika ngazi mbalimbali za elimu ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu nchini.

Maboresho haya yalitokana na ukweli kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi na kuendelea na elimu ya sekondari kutokana na Sera ya Elimu bila Malipo.

Pamoja na kazi hiyo nzuri bado kuna uhitaji katika elimu ya Awali na Msingi na ndio maana Serikali imekuja na Mradi wa BOOST ambao unakwenda kuboresha upatikanaji wa fursa sawa katika ujifunzaji bora wa Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara.

Ni vema kuipongeza Serikali kwa kuja na mradi huu kwa kuwa utasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi wa elimu ya awali na msingi darasani kutokana na ujenzi wa vyumba vya madarasa. Pia ujenzi wa matundu ya vyoo utasaidia wanafunzi kusoma katika mazingira bora.

Pia utasaidia wanafunzi kumudu Stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa kuwa walimu watajengewa uwezo katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na kununuliwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunzi.

Pia Mradi utaweka mazingira bora, salama na rafiki pamoja na huduma muhimu za jamii zikiwemo umeme, maji safi na salama na sehemu za kunawia mikono na kuchangia upatikanaji wa huduma ya elimu na hivyo wanafunzi kubaki shuleni muda wote wa masomo.

Utekelezaji wa Mpango wa shule salama utakaoambatana na mafunzo kwa walimu kuhusu malezi bora kwa wanafunzi, uzingatiaji wa maadili ya kazi na ufundishaji unaozingatia ushirikishaji wa wanafunzi wa jinsia zote, uimarishaji wa elimu ya ushauri nasaha na unasihi, uimarishaji wa elimu na stadi za maisha na utatuzi wa changamoto za maisha kwa wanafunzi.

Mradi pia utasaidia kupunguza vihatarishi vinavyochangia wanafunzi kuacha shule kwa kuimarisha mawasiliano kati ya uongozi wa shule, walimu, wazazi/walezi na jamii ikiwa ni pamoja na kuimarisha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji, kuimarisha Maktaba mtandao na mfumo wa usimamizi katika ujifunzaji

Mradi huu ni sehemu ya Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu Awamu ya Pili (EP4R II) na inachangia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya elimu wa miaka mitano 2021/22 hadi 2025/26 na unasimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).



Miundombinu >

# Serikali yafanya Maboresho Makubwa Miundombinu Vyuo vya Ualimu

Zaidi ya Shilingi bilioni 39.7 zimetumika kuboresha Miundombinu ya Vyuo vya Ualimu vinne ili kuviwezesha kuandaa walimu watakaofundisha vijana ili wapate ujuzi wa kuwawezesha kuingia katika soko la ajira.

Akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki, mara baada ya kuzindua Miundombinu iliyojengwa na iliyokarabatiwa katika Vyuo vya Ualimu vinne nchini, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema lengo kubwa la kujenga na kukarabati miundombinu hiyo ni kuondoa changamoto ambazo zimekuwa zikitolewa na wananchi kuhusu elimu inayotolewa kwa vijana.



Mhe. Rais ameongeza kuwa wananchi wamekuwa wakilalamika kwamba elimu inayotolewa haitoi ujuzi wa kuwawezesha kuingia katika soko la ajira iwe kwa kuajiriwa ama kujiajiri.

"Wananchi mmekuwa mkilalamika kwamba tunawachukua vijana wenu na kukaa nao kwa miaka mingi na tunawarudisha na karatasi tu ambazo haziwapi uwezo wa kuajiriwa ama kujiajiri kwa kuwa hawana ujuzi ambao wameupata katika miaka yote, hivyo maboresho haya yanalenga kutatua changamoto hii" amesema Mhe Rais.

Ameongeza kuwa ujenzi na ukarabati wa miundombinu hiyo unakwenda sambamba na maboresho ya mitaala na mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 yanayotupeleka katika elimu ujuzi.

Aidha, ameishukuru serikali ya Canada kwa ufadhili wa mradi huo uliojenga na kukarabati miundombinu hiyo , huku akiipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa usimamizi mzuri wa Mradi huo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof Adolf Mkenda amemwambia Mhe. Rais kuwa Mradi huo umetekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Canada ambapo Serikali ya Canada imetoa jumla ya Sh. 30,952,925,648.41 na Serikali ya Tanzania imetoa Kiasi cha Sh. 8,846,876,095.43.

Kiongozi huyo ameongeza kuwa ukarabati huo umefanyika katika vyuo vya ualimu vya vinne ambavyo ni Chuo cha Ualimu Mpuguso Mbeya, Chuo cha Ualimu Kitangali Mtwara, Chuo cha Ualimu Ndala Tabora na Chuo cha Ualimu Shinyanga ambapo vyote vimejengewa mabweni, madarasa, bwalo, maktaba, maabara na mifumo ya maji safi na kwamba maboresho hayo yameongeza udahili wa walimu tarajali na kuviwezesha kutoa mafunzo ya elimu ujuzi.

"Mhe. Rais pamoja na Mapitio ya Sera na mabadiliko ya mitaala, suala la ukarabati wa vyuo vya ualimu ni muhimu sana kwa kuwa walimu wanaotoka katika vyuo hivi wanatarajiwa kwenda kuwafundisha na kuwaandaa vijana wa kitanzania kwa kuwapatia mafunzo yanayolenga kutoa elimu ujuzi na mfano Chuo hiki cha Mpuguso kitatoa elimu ya kilimo na ufugaji kwa walimu tarajali" amesema Prof Mkenda

Aidha, ameongeza kuwa rasimu ya Mitaala inayozingatia agizo la Mhe. Rais la kutoa elimu ujuzi pamoja na Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 itakamilika karibuni na kwamba wizara itakuwa na Kongamano kubwa la elimu Mwezi Oktoba mwaka huu kujadili na kutoa maoni katika rasimu hizo ambapo Rais anatarajiwa kufungua Kongamano hilo.

Naye Balozi wa Canada nchini Balozi Hellen Fytche amesema Serikali ya Canada itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha inaboresha upatikanaji wa elimu bora katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu katika vyuo vya ualimu ili kuviwezesha kutoa walimu wenye uwezo wa kutoa elimu ujuzi.

Amesisitiza kuwa Serikali ya Canada inaamini maboresho hayo yatasaidia kufikia lengo namba nne la Maendeleo endelevu ambalo linataka kuhakikisha elimu jumuishi na linganifu inatoa fursa za kujifunza kwa usawa na kwa wote.

Serikali inamiliki vyuo vya ualimu 35 ambapo vyuo hivyo vingi vilijengwa miaka mingi iliyopita na kufanya miundombinu yake kuwa chakavu, hivyo mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha vyuo hivyo vyote vinafanyiwa ukarabati mkubwa na kuwa na miundombinu stahiki kulingana na mazingira ya sasa.



## Uwekezaji Elimu Ujuzi >




# Tutaendelea kuwekeza katika Elimu Ujuzi

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali ya Awamu ya Sita imejizatiti katika kutoa elimu ujuzi na hivyo itaendelea kuwekeza katika elimu ya ufundi ikiwemo ujenzi wa Vyuo vya VETA katika kila wilaya na Mikoa.

Amesema hayo baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Mbarali kinachojengwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia chini ya Mradi wa Kukuza Ujuzi (ESPJ).

Ametumia nafasi hiyo kuwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya na hususan Wilaya ya Mbarali kuhakikisha wanakitumia chuo hicho kupata ujuzi kulingana na shughuli zao za kiuchumi.

"Najua hapa kuna vijana wengi mna shughuli mbalimbali tumieni sana chuo hiki kupata ujuzi na kuongeza tija katika kazi zenu na hata kuanzisha viwanda vya uchomeleaji na vingine," amesema Mhe. Samia

Akimkaribisha Rais Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amesema ujenzi wa chuo hicho umefikia asilimia 95 na kwamba hadi kukamilika utatumia Shilingi Bilioni 2.7.

Ameongeza kuwa Chuo hicho kinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba mwaka huu na kuanza kudahili wanafunzi wa kozi fupi wapatao 240 na wanafunzi wa kozi za muda mrefu wapatao 500 mwezi Januari 2023.

Mhe. Mkenda amemshukuru Rais kwa kuongeza uwekezaji kwa ajili ya ujenzi wa VETA kupitia bajeti ambapo Bilioni 100 zimetengwa kwa ajili hiyo.

Chuo cha VETA Mbarali ni sehemu ya Vyuo 25 vya Wilaya na vinne vya Mikoa vinavyojengwa kupitia mradi huo ambao unaogharimu takriban Bilioni 49. Aidha ampongeza Rais kwa kutoa fedha za Mpango wa Mapambano dhini ya Uviko na Ustawi ambazo pia zime changia katika kukamilisha vyuo hivyo.

Mkenda ameeleza kuwa Wizara kwa sasa inafanya tathmini ya kujua uwezo wa wanafunzi wanaotoka VETA katika kazi na uwezo wa kuajiriwa kwao kupitia waajiri mbalimbali. Lengo ni kuhakikisha elimu inayotolewa ni bora na sahihi kulingana na uhitaji wa soko pamoja na kuongeza kasi ya kuandaa Walimu wa Ufundi.

"Mhe Rais katika fedha za Uviko tumewekeza katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Morogoro na pale Chuo cha Ufundi Arusha. Lengo letu ni pamoja na kasi ya kuongeza Vyuo wawepo walimu wa ufundi wa kutosha" amesema Mhe. Mkenda

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa VETA CPA Anthony Kasore amesema Vyuo vyote vya VETA vya Wilaya vinatoa kipaumbele katika mafunzo yanayoendana na shughuli za kiuchumi za Mkoa na Wilaya husika huku akitolea mfano Chuo cha Mbarali ambacho kitatoa mafunzo ikiwemo uchomeaji, ufundi mitambo, kompyuta, ukatibu muhtasi, ushonaji na umeme wa majumbani.



Ufumbuzi Changamoto >

# Mwanafunzi NMIST aja na suluhisho kwa wakulima wa soya

Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela imekuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu inayolenga kusaidia jamii na kukuza viwanda kupitia tafiti na bunifu zinazofanywa na wanafunzi wa Taasisi hiyo.

Hayo yamejidhihirisha kupitia Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu (PhD) ya Kilimo Endelevu wa Taasisi hiyo Bi. Monica Nakei ambae anafanya utafiti wa mbolea asilia itokanayo na vimelea vya bakteria jamii ya rhizobia.

Akizungumza katika maonesho ya 28 ya Nanenane Kanda ya Kaskazini yanayoendelea viwanja vya Themi Arusha Agosti 2, 2022 Mwanafunzi huyo amesema amefanya utafiti wa mbolea hiyo kupitia zao la soya na kwamba utafiti ukatapokamilika mbolea hiyo itakuwa tayari kwa matumizi.

Amesema katika utafiti wake amegundua kuwa mbolea hiyo ina faida nyingi ikiwemo kuongeza virutubisho vya nitrogeni na fosforasi kwa mimea ya Soya na kuimarisha afya ya udongo na kuweka usawa katika mfumo wa ikilojia ya udongo.

Bi. Monica ameeleza kuwa, faida nyingine ni pamoja na mazao yatokanayo na mbolea hiyo kutokuwa na kemikali zenye kuleta madhara kwa walaji na gharama yake ni nafuu kwa wakulima.

"Nawashauri wakulima wa soya (soyalishe) kutumia mbolea asilia ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo kwani mbolea hii pamoja na kuwa na thamani kwenye zao lenyewe inatunza mazingira kama maji, hewa na udongo,"amesema Mwanafunzi Monica.

Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela inashirikia maonesho ya 28 ya NaneNane yanayoendelea katika viwanja vya Themi jijini Arusha ambapo kupitia wanafunzi wake inaendelea kutoa elimu ya migomba iliyoboreshwa, kiatilifu biologia cha kudhibiti wadudu katika zao la Kabeji, upimaji wa udongo , chakula cha samaki chenye lishe, buheri wa Afya,Nutrano,NUSA,Omega -3DHA,Ngwara,Kweme na vyakula visivyo vya kemikali.



Teknolojia>



# DIT yatakiwa kuhamisha teknolojia kutoka nje ya nchi

Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) imetakiwa kuendelea kuhamisha teknolojia kutoka nje kwa kupeleka wataalam nje ya nchi kujifunza na kualika wataalam kutoka nje ili kama nchi kutengeneza bidhaa ambazo kwa sasa zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Hayo yameelezwa jijini Dar es Salaam na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (Mb) alipotembelea Taasisi hiyo kuona kiwanda cha uzalishaji wa vipuri vya bajaji, pikipiki na magari ambacho kinatumika kama darasa kwa wanafunzi wa taasisi hiyo.

Amesema kwa kuwa na utaratibu wa kupelekea wataalamu nje kujifunza ni kuendelea kujinoa zaidi kwenye teknolojia ambazo zitasaidia katika utendaji.

Akizungumzaia uzalishaji wa vipuri unaofanyika DIT amesema kwa sasa ni hatua ya awali lakini kwa baadae Taasisi hiyo itaweza hata kuzalisha pikipiki.

"Tukiendelea hivi, baadae tunaweza kusema tuzalishe pikipiki zetu, wenzetu India na China walianza hivihivi kabla ya kuanza kutengeneza pikipiki na magari, leo mnatengeneza vipuri baadae tutaweza kutengeneza pikipiki zetu," amesema Waziri Profesa Mkenda.

Waziri Mkenda ameahidi kumualika Mhe. Kassim Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufungua kiwanda hicho kutokana na kuona uzalishaji wa vipuri unaofanyika katika kiwanda hicho na umuhimu wa bidhaa hizo kwenye jamii.

Aidha, ameupongeza uongozi wa Taasisi hiyo kwa kuendelea kubuni vitu mbalimbali ambavyo vitakuwa msaada kwa vijana kupata ajira na pia taifa kwa ujumla kwani itasaidia kuokoa fedha nyingi za kigeni ambazo hutumika kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, (DIT) Mhandisi Dkt. Richard Masika amesema Taasisi hiyo kwa sasa imepiga hatua ambayo ni ya kutoa elimu kwa wanafunzi wao ambayo itawawezesha kuajiriwa kwa wingi pamoja na kujiajiri.

" Kwa muda mrefu DIT imekuwa ikitoa elimu kwa nadharia zaidi baada ya hapo ikaweka msisitizo mkubwa kwa vitendo lakini tukagundua pamoja na kufanya hivyo bado wahitimu wamekuwa wanaajirika lakini hawawezi kujiajiri, sasa tumeamua kutengeneza mazingira ya kiwanda, wanafunzi wafanye kazi za uzalishaji kwenye kiwanda hatua kwa hatua na zile bidhaa zinazotoka zinakwenda kutumika," amesema Dkt. Masika.

Aidha, amesema kwa mwaka huu DIT imejiwekea malengo ya kuzindua viwanda viwili ambavyo vitazinduliwa mwezi Disemba mwaka huu, viwanda hivyo ni hicho cha vipuri kilichopo kampasi Kuu ya Dar es Salaam na cha bidhaa za ngozi kitakachokuwa Kampasi ya Mwanza.

Naye Mkuu wa Taasisi hiyo, Profesa Preksedis Ndomba amesema vipuri vinavyozalishwa katika Taasisi hiyo vinatengenezwa kwa kutumia chupa za plastiki zilizokwishatumika ambazo huyeyushwa na kutengeneza pallets ambazo zinasaidia kutengeneza vipuri hivyo ambavyo hutumika kwenye pikipiki,bajaji na kwenye magari.

Miundombinu >

# Shule zenye changamoto ya miundombinu kunufaika na Mfuko wa Elimu

- **Bilioni 8.9 kutumika katika mwaka wa fedha 2022/23**
- **Milioni 500 kati ya hizo kunufaisha Taasisi za elimu ya juu Tanzania Visiwani**




Shule zenye uhaba mkubwa wa miundombinu unaotokana na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi na zilizosajiliwa zinatarajia kunufaika na Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Hayo yameleezwa Jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa mikutano wa Idara ya Habari - MAELEZO kuhusu utekelezaji na mwelekeo wa Bajeti ya TEA kwa mwaka 2022/23.

Amesema TEA imepanga kutumia kiasi cha Sh. Bilioni 8.9 kwa ajili ya kufadhili miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu nchini kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa ambapoTaasisi mbili za elimu ya juu za Tanzania Zanzibar pamoja na shule zilizo na changamoto za miundombinu zitanufaika.

Ametaja Taasisi za elimu ya juu zitakazonufaika kuwa ni Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Zanzibar (KIST) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ambapo jumla ya Sh Milioni 500 zitatumika.

"Tunaendeleza jitihada za Serikali kuwezesha upatikanaji wa elimu bora kwa usawa nchini, tutatumia Sh bilioni 8.9 kwa ajili hiyo na kujenga jumla ya miradi 96 katika shule za msingi na sekondari Tanzania bara pamoja na Taasisi mbili za elimu ya juu Tanzania Zanzibar. Shule zitakazonufaika ni zenye vigezo ambavyo vimetajwa pamoja na kuwepo kwenye kanzi data ya TEA," amesema Bibi Geuzye

Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa 99, matundu ya vyoo 792, maabara 10 za masomo ya sayansi kwa ajili ya shule tano za sekondari, nyumba za walimu 52 na mabweni 10.

Miradi mingine ni ujenzi wa miundombinu ya wanafunzi wenye mahitaji maalum inayojumuisha madarasa 10, matundu ya vyoo 40 pamoja na mabweni mawili katika shule sita zenye watoto wenye mahitaji maalum.

Awali Mkurugenzi Geuzye alisema TEA katika mwaka wa fedha 2021/2022, ilitumia kiasi cha Sh. Bilioni 8.6 kufadhili miradi 160 ya kuboresha miundombinu ya elimu katika shule 151 nchini. Miradi hiyo ilijumlisha ujenzi wa madarasa 210 katika shule 70, Maabara 2 za sayansi katika shule za sekondari zenye mahitaji maalum, Matundu ya vyoo 1920 katika shule 80, vifaa vya kujifunzia na kufundishia na uendelezaji wa miundombinu katika shule tisa za watoto wenye mahitaji maalum pamoja na ofisi mbili za walimu katika shule mbili.

Aidha Mkurugenzi Geuzye ameendelea kuhimiza wadau wa elimu kutoa ufadhili wa miradi ya elimu kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao una jukumu la kisheria la kuratibu michango inayotolewa katika sekta ya elimu nchini ili kuwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi za wachangiaji na thamani ya michango.

"Taasisi au watu wanaochangia kupitia TEA wanatambuliwa rasmi kwa kupewa cheti maalum na wanaweza kuomba nafuu ya kodi kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato Nchini (TRA). Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001 na Kifungu cha 16 cha Sheria ya Mapato ya mwaka 2006," alisema Mkurugenzi Geuzye.

Kuhusu utekelezaji wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF), Mkurugenzi Mkuu wa TEA amesema hadi kufikia mwezi Juni 2022 kiasi cha Shs Bilioni 9.7 zinatumika kufadhili miradi 81 ambapo jumla ya wanufaika 33,510 ikiwa ni wanaume 17,257 (51.5%) na wanawake 16,253 (48.5%) wamepatiwa mafunzo.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya umma inayofanya kazi chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. TEA inaratibu Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao unasaidia jitihada za Serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu kwa lengo la kuongeza ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa. Pia TEA inaratibu Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia.

ElimuMsingi >

# Utekelezaji wa Makubaliano ya Ushirikiano kwenye ElimuMsingi kati ya Tanzania na Afrika Kusini waanza

Utekelezaji wa Hati ya Makubaliano ya ushirikiano kati ya Tanzania na Afrika Kusini kwenye maeneo mbalimbali ya elimumsingi umeanza kwa kasi ambapo Julai 28, 2022 Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda alishuhudia uwekaji saini wa rasimu ya Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Makubaliano.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mara baada ya kushuhudia tukio hilo waziri Mkenda amesema hatua hiyo inatoa mwelekeo wa jinsi ya ushirikiano baina ya nchi hizo mbili kwenye elimu utatekelezwa.

"Baada ya kusaini Hati ya Makubaliano Julai 7, 2022 tulikubaliana na Waziri mwenzangu anayeshughulika na ElimuMsingi nchini Afrika Kusini kwamba tusiwe na hati ya makubaliano tu halafu tukaiweka kabatini, timu zikutane kuweka mpango kazi wa utekelezaji," amesema Prof. Mkenda

Alisema kikubwa kwenye makubaliano hayo sio kufundisha kiswahili tu lakini kuweka msukumo katika kuendeleza kiswahili katika Bara la Afrika.

Alisema Tanzania ina wajibu mkubwa wa kukuza kiswahili na kuhakikisha kinasambaa katika nchi zote Afrika.

Ujumbe wa wataalamu kutoka Wizara ya ElimuMsingi ya Afrika Kusini pia umetembelea shule ya Msingi Chief Albert Luthuli iliyopo Mazimbu Mkoani Morogoro.

Shule hii iko katika moja ya eneo waliloishi wapigania Uhuru wa Afrika ya Kusini wakati wa harakati za ukombozi wa nchi hiyo.

Akiwa Shuleni hapo Mkuu wa Msafara huo, Enoch Rabotapi ambaye ni Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Elimu ya Ualimu nchini humo (Chief Director Teacher Development) ameahidi ushirikiano kati ya shule hiyo na baadhi ya shule zitakazobainishwa nchini Afrika Kusini kwa kubadilishana uzoefu na walimu.

"Uhusiano wa nchi ya Tanzania na Afrika ya Kusini ni wa muda mrefu, na itakumbukwa mwaka 2018 Rais wetu wa Afrika Kusini akiwa nchini Tanzania aliahidi kutembelea shule hii. Na hivi juzi Mwezi huu wa Julai Waziri wetu wa Elimu ya Msingi nae alitoa ahadi na ndio maana tupo hapa. Tumefurahi kwa kweli, kikubwa tunaahidi kushirikiana kuendeleza shule hii," amesema Mkurugenzi huyo.

Akizungumza kabla ya kuanza ziara katika Shule hiyo Sylvia Lupembe, Mkuu wa Mawasiliano Serikalini Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia amesema Ujumbe huo uko nchini kuungana na watalaamu wa elimu wa hapa nchini na wa Kiswahili kwa ajili kuandaa Mpangokazi wa Utekelezaji wa Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika kuendeleza elimumsingi ikiwemo ufundishaji Kiswahili nchini Afrika Kusini.

Hati hiyo ilisainiwa na Mawaziri wa Elimu wa nchi hizo mbili Jijini Dar es Salaam Julai 7, 2022 ambayo ilikuwa Siku ya Kiswahili Duniani.





Uboreshaji Elimu >

# Maoni Lugha ya Kufundishia: Kipaumbele katika mapitio ya Sera ya Elimu



Wito umetolewa wa kufanya tathmini ya kutosha juu ya lugha itakayokubalika kufundishia hasa kwa upande wa walimu na wanafunzi katika ngazi zote za Elimu nchini.

Wito huo umetolewa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Mwanahamisi Ameir wakati akifungua kikaokazi cha maoni ya uchambuzi na tathmini ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kinachofanyika Zanzibar.



Amesema kuwa matayarisho ya walimu upande wa mafunzo ni ya muhimu katika kuhakikisha walimu wapya wanaozalishwa na ambao wapo tayari kazini wanakuwa na vigezo vinavyotakiwa.

"Matayarisho ni ya muhimu kujua vitu kama sifa za wanaoenda kusomea ualimu, sifa za vyuo, muda wa mafunzo uweje, matayarisho ya walimu kumudu lugha husika ya kufundishia, vyote hivi vitolewe kwa kiwango katika vyuo vyote ili kupata walimu wenye sifa stahiki," amefafanua Ameir.

Akiongea katika kikao hicho, Mwenyekiti wa timu ya Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Prof. Joseph Semboja amesema lengo la kikaokazi hicho ni kupokea maoni kutoka kwa wadau wa elimu kutoka upande wa Zanzibar juu ya maboresho ya Sera hiyo.

Kikaokazi hicho kimehudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo, Jinsia, Wazee na Watoto, Abeda Rashid Abdallah na wadau mbalimbali wa Elimu kutoka Bara na Kisiwani humo.

Mikopo Elimu ya Juu / Michezo >

# Serikali kuhakikisha hakuna upendeleo utoaji mikopo kwa wanafunzi Elimu ya Juu

Serikali imejipanga kuhakikisha mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu inatolewa kwa wanafunzi bila upendeleo ama mashinikizo kwa kuunda tume ya wataalamu kuangalia utaratibu unaotumika na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa sasa.

Hayo yamesemwa jijini Dar es Salaam na Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wakati akiongea na Wahariri pamoja na waandishi wa habari kuhusumwelekeo wa Wizara, Vipaumbele na Maeneo ya Kimkakati katika Utekelezaji wa wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

Prof. Mkenda amesema tume iliyoundwa itahakikisha vigezo vinafuatwa katika kutoa mikopo na kuwataka wanafunzi kufuata taratibu hizo ili kupunguza changamoto zinazotokana na makosa yanayojitokeza wakati wa ujazaji wa taarifa.

"Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na bodi sasa hivi katika kuratibu mikopo hiyo nimeunda tume ya wataalamu watatu, inaongozwa na Prof. Allen Mushi, ni Profesa wa hisabati na mtaalamu wa mifumo, atasaidiwa na Mwanaidi Makame mtaalam wa kompyuta na mifumo pamoja na Dkt. Martin Chegele ambaye ni mtaalamu wa kufanya tathmini," alisema Prof Mkenda.

Ameongeza kuwa lengo la kuunda tume hiyo ni kuhakikisha mikopo inatolewa kwa haki kwa kila anayestahili kupata, aidha aliwataka watanzania kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa iwapo kuna wanafunzi wanaopata mkopo kwa udanganyifu na kupelekea wanaostahili kukosa.

Profesa Mkenda aliongelea pia suala la Serikali kuwahamasisha wanafunzi kuchukua masomo ya sayansi kwa kutoa zawadi kwa wale waliofaulu vizuri sana kuendelea na masomo hayo kwa ngazi za juu.

# Idadi ya Vyuo vya Ualimu vinavyofundisha Somo la Michezo vyaongezeka

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeongeza idadi ya Vyuo vya Ualimu vinavyofundisha somo la michezo na kufanya vyuo hivyo kuwa sita kutoka vinne vilivyokuwa vinatoa mafunzo hayo.



Hayo yamesemwa Mkoani Tabora na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Francis Michael wakati akifungua Mashindano ya kitaifa ya Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari (UMISSETA).

Dkt Michael ameeleza kuwa hatua hiyo ni kutekeleza agizo la Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilolitoa Mkoani Mtwara Juni 08, 2021 wakati wa Ufunguzi wa Mashindano ya UMISSETA na Agosti 04, 2022 Mkoani Tabora wakati wa ufunguzi wa UMITASHUMTA ambapo aliagiza kuwa Vyuo vyote vya Ualimu viandaliwe kufundisha somo la Michezo ili walimu watakaohitimu katika vyuo hivyo waweze kufundisha somo hilo katika shule zote za Msingi na Sekondari.

Ametaja Vyuo vya Ualimu vinavyofundisha somo la michezo kwa sasa kuwa ni Ilonga, Butimba, Mpwapwa,Tarime, Tabora na Mtwara Kawaida na kwamba Mpango wa Serikali ni kuwezesha vyuo vyote vya ualimu nchini kutoa elimu ujuzi ikiwemo Michezo na sanaa ili kuandaa walimu wenye stadi na ujuzi.

"Zaidi ya michezo pia tutatoa ujuzi wa kilimo, ufugaji na ufundi. Nitoe wito kwa vyuo vya ualimu nchini kujipanga katika utekelezaji huo," amesema Katibu Mkuu Michael

Aliongeza kuwa kwa sasa Wizara inafanya mapitio ya mitaala ya elimu na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 lengo ni kuhakikisha kunakuwa na mitaala itakayomuandaa muhitimu kupata maarifa, ujuzi na stadi na kwamba wale wenye vipaji vya michezo waweze kuandaliwa mazingira wezeshi kumudu stadi hizo iliwaweze kupata ajira kupitia vipaji hivyo.

Pia Wizara inapitia mapendekezo ya TAHASUSI za Kidato cha Tano na Sita zinazojumuisha masomo ya Sanaa na Michezo ili wanafunzi waweze kuendeleza Stadi zao walizozipata walipojifunza somo la Elimu kwa Michezo walipokuwa kidato cha Kwanza hadi cha Nne.

Akizungumzia mashindano ya UMISSETA kwa mwaka 2022 Katibu Mkuu Michael amesema imejumuisha michezo ya Mpira wa Miguu wanawake na wanaume, Netiboli, Mpira wa Kikapu wanawake na wanaume, Mpira wa Wavu wanawake na wanaume, Mpira wa Mikono wanawake na wanaume, Riadha wanawake na wanaume, Mpira wa Meza wanawake na wanaume.

Pia imehusisha Sanaa za Maonesho ambazo ni Ngoma, Kwaya na Muziki wa Kizazi Kipya kwa wanawake na wanaume ambapo jumla ya wanamichezo 4200 wameshiriki.

Uimarishaji Ujifunzaji>



# Mradi wa BOOST kuimarisha Ujifunzaji wa Elimu ya Awali, Msingi

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inatekeleza Mradi wa kuimarisha Ujifunzaji katika Elimu ya Awali na Msingi ***(Boosting Student Learning Outcomes)*** wenye lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara.

Mradi wa BOOST ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu Awamu ya Pili (Education Program for Results – EP for R II) ambapo unatekelezwa kwa mkopo wa riba nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB) wenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni Mia Tano (US $500 Mil.) na utatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2025/26.

> "Mradi utasaidia kuongeza uwiano wa uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya Awali kutoka asilimia 76.9 hadi asilimia 85 na kwa Halmashauri zilizo katika kundi la robo ya chini kutoka asilimia 57.5 hadi kufikia 65.6.

Mradi huo utaongeza fursa za upatikanaji wa elimu kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule za Awali na Msingi, uwezo na umahiri wa walimu katika ufundishaji na ujifunzaji darasani pamoja na kuimarisha usimamizi wa fedha, utawala bora na utoaji wa huduma za elimu.

Kupitia Mradi huo vitajengwa vyumba vipya vya madarasa 12,000 na kuwekewa vifaa, Shule za Msingi 6,000 kuwezeshwa kutekeleza Programu ya Shule ya msingi Salama (Safe School Program) na kuboresha madarasa 12,000 ya Elimu ya Awali pamoja na njia bora za ufundishaji vikiwemo vifaa vya kujifunzia.

Pia mradi utasaidia kuongeza uwiano wa uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya Awali kutoka asilimia 76.9 hadi asilimia 85 na kwa Halmashauri zilizo katika kundi la robo ya chini kutoka asilimia 57.5 hadi kufikia 65.6.

Ushiriki wa walimu katika Mpango wa Mafunzo endelevu kazini ni moja ya matokeo ya mradi ambapo utasaidia ushiriki huo kufikia asilimia 50. Pia kutakuwa na ongezeko la asilimia 50 ya wanafunzi wa darasa la pili kufikia kiwango cha chini cha kumudu stadi za Kusoma na Kuandika na asilimia 35 katika Kuhesabu.

Mengine ni kuongezeka kwa kiwango cha wanafunzi kubaki shuleni katika Halmashauri zilizo katika kundi la robo ya chini kutoka asilimia 55.9 hadi asilimia 66.24, Umahiri wa matumizi ya TEHAMA kwa walimu na wanafunzi na kuimairisha Maktaba Mtandao na Mfumo wa usimamizi katika ujifunzaji.

## NUKUU >

**"TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA"**

***– Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***
***Bungeni - April, 2021***

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifala Elimu ya Ufundi (NACTE),**
S.L.P 7109, DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P. 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz